

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

Anwani ya simu: Hazina, Dodoma,  
Simu Nambari: +255-26-2160000,  
**Telefax: 41329**  
Nukushi : +255-26-2963109,  
Barua pepe: [ps@hazina.go.tz](mailto:ps@hazina.go.tz)  
Tovuti: [www.mof.go.tz](http://www.mof.go.tz)



Mji wa Serikali – Mtumba,  
Mtaa wa Hazina,  
Sanduku la Barua 2802,  
**40468 DODOMA,**  
**TANZANIA.**

### TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUIDHINISHWA KWA FEDHA ZA MKOPO NAFUU WA KUKABILIANA NA ATHARI ZA UVIKO-19 KUTOKA IMF

**DODOMA: Tarehe 8 Septemba, 2021:** BODI ya Wakurugenzi ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) limeridhia kutoa mkopo nafuu kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wa jumla ya dola za Marekani milioni 567.25 sawa na shilingi triliuni 1.3 kwa ajili ya kukabili ana na athari za UVIKO-19.

Fedha hizo zinajumuisha mkopo nafuu usio na riba kuitia dirisha la *Rapid Credit Facility (RCF)* wa jumla ya dola za Marekani milioni 189.08; na mkopo nafuu wenyre riba ndogo kuitia dirisha la *Rapid Financing Instrument (RFI)* wa dola za Marekani milioni 378.17.

Fedha hizo zitatumika ndani ya mwaka huu wa fedha katika kukabili ana na athari za kiuchumi na kijamii zitokanazo na UVIKO-19.

Sekta zitakazonufaika kulingana na makubaliano yetu na IMF ni afya, elimu, utalii, maji, pamoja na kusaidia kaya maskini kuitia mfuko wa hifadhi ya jamii (TASAF) na kuwezesha makundi maalum ya vijana, wanawake na wenyre ulemavu.

Kila sekta itatumia fedha hizo kwenye masuala yanayolenga kukabili ana na athari za UVIKO-19 ambapo pamoja na mambo mengine, Sekta ya afya itanunua dawa na vifaa tiba vya kupambana na UVIKO-19 na kugharamia utekelezaji wa mpango wa chanjo.

Sekta ya elimu itaweka mazingira yatakayowezesha wanafunzi kujifunza bila msongamano na kuchukua tahadhari ya maambukizi ya UVIKO-19 ikiwa ni pamoja na ujenzi wa maboma ya shule na kuongeza madawati.

Sekta ya maji itaongeza miundombinu ya maji itakayowezesha upatikanaji wa huduma ya maji tiririka kwa wingi zaidi mijini na vijijini; na Mpango unaoendelea wa TASAF utaongezewa fedha (Complement) ili kusaidia kaya maskini zilizoathirika na UVIKO 19.

Aidha, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) itawezeshwa pia kukabili ana na athari za UVIKO-19 katika sekta zilizoathirika ikiwa ni pamoja na afya, utalii na kilimo.

Waziri mwenye dhamana ya Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchomba (Mb), ameziasi sekta zote zitakazopata fedha hizi kuzitumia kulingana na Mpango tulioandaa kwa pamoja na sekta husika wa kukabili ana na athari za UVIKO-19 – *Tanzania COVID-19 Socio-Economic Recovery and Response Plan (TCRP)*. Aidha, fedha hizo zitumike kwa kuzingatia makubaliano yetu na IMF kama ilivyoainishwa kwenye barua ya dhamira ya Serikali (Letter of Intent - LOI) ikiwa ni pamoja na utoaji wa taarifa za utekelezaji kwa wakati.

Imetolewa na:

Benny Mwaipaja  
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini  
WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO